# Usilimishaji wa Vielelezo katika Fasihi ya Watoto: Mfano kutoka *Wasifu wa Mwana Kupona* (2008) na *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (2015)

Stephen M. Mwendwa, Pamela M.Y. Ngugi na Catherine Ndungo
Chuo Kikuu cha Kenyatta

**Ikisiri**

Makala hii inachunguza usilimishaji[1] wa vielelezo vilivyotumika katika hadithi ya *Wasifu wa Mwana Kupona* (King'ei, 2008) na *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (Hadjavayanis, 2015) na mchango wake katika kuendeleza ujumbe. Tafiti chache za usilimisho wa vielelezo katika hadithi za watoto zimefanywa (taz. Muthubi, 2005; Kaui, 2011; Sohaimi, 2011; Balodis, 2012; Ratiba, 2014; Omuya, 2017). Hata hivyo, tafiti hizi za awali hazijahusisha moja kwa moja hadithi ya *Wasifu wa Mwana Kupona* (2008) na *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (2015). Ni katika msingi huu ndipo makala imeshughulikia aina za vielelezo vilivyotumika katika hadithi teule na mchango wake katika kuendeleza ujumbe. Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Usilimisho ya George Bluestone (1957) na baadaye ikaendelezwa na Goodman (1976), Andrew (1984) na Starrs (2006). Nadharia ya Usilimisho inahusu uzalishaji wa kazi nyingine huru baada ya kazi ya awali kuzalisha kazi nyingine. Data iliyotumika katika makala hii imetokana na kusoma machapisho mbalimbali maktabani kama vile majarida, tasnifu na vitabu. Vilevile, usomaji, uchambuzi na hata unakili wa vipengele muhimu vinavyohusiana na masilimisho teule ulifanywa. Matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba aina za vielelezo vilivyotumika katika hadithi teule ni vibonzo, ramani, picha zilizotiwa rangi na michoro. Aidha, imebainika kuwa vielelezo vinaweza kutumika kupasha ujumbe iwapo vitatumika ipasavyo.

## 1.0 Utangulizi

Ni vigumu kupata maana ya moja kwa moja iliyotumika kuifafanua dhana ya usilimishaji katika mawanda ya kifasihi ulimwenguni. Hivyo, kuna wataalamu mbalimbali ambao wameifasili dhana hii kulingana na malengo yao hivi kwamba, kuna wale wanaofupisha tu dhana hii, wanaoirekebisha na wanaoitafsiri (taz. Vinay na Darbelnet, 1958; Klingberg, 1986; Shavit, 1986; Newmark, 1988; Oittinen, 2000; Baker, 2001; Sanders, 2006, miongoni mwa wengine). Vinay na Darbelnet (1958) wanaeleza kuwa usilimishaji ni hatua ya saba katika taratibu za tafsiri, ambayo hutumika tu wakati matini chasili inayorejelewa haipo katika utamaduni wa

[1] Linalotokana na neno la Kiingereza 'assimilation'.

*Kioo cha Lugha 2020, 18: 114-129*

hadhira lengwa. Fasili ya Vinay na Darbelnet inafanana na fasili za wataalamu wengine kama vile Baker (2001) na Brisset (1990), ambao wanasema kuwa usilimishaji unahusu kutafsiri matini chasili ili kuipa matini hiyo tafsiri mpya huku vipengele kama vile lugha, wahusika na tamaduni vikibadilishwa ili kuondoa uchangamano wa matini hiyo. Klingberg (1986) anasema kuwa usilimishwaji kwa ujumla unamaanisha hali ya kufasili sura mbalimbali za lugha chasili hadi lugha lengwa. Wakati wa kufasili sura mbalimbali za lugha chasili ni lazima mwandishi azingatie majukumu ya lugha lengwa katika lugha chasili. Hivyo, lazima kuwapo na uhusiano kati ya lugha hizo mbili.

Newmark (1988) anaeleza kuwa usilimishwaji ni mojawapo ya mbinu-huru ya tafsiri. Katika utafsiri wa aina hii, mwandishi huwa analazimika kuhifadhi ploti ya matini chasili. Hata hivyo, vipengele vingine vya fasihi kama vile lugha, wahusika na utamaduni vinaweza kubadilishwa ili kuwafikia wanaolengwa. Kuna uhusiano wa karibu kati ya usilimishaji na utafsiri kwa mujibu wa fasiri hii kwa sababu, wakati wa usilimisho wa kiuaminifu mwandishi huhifadhi vipengele vingine kama vile ploti, wahusika na maudhui. Naye Oittinen (2000) anaeleza kuwa usilimishaji ni marekebisho ya kifasihi yanayofanyiwa matini chasili ili iweze kutumika na hadhira ya watoto. Oittinen anapendekeza kuwa, wakati mwandishi anaposilimisha kazi ili iweze kusomwa na hadhira ya watoto, analazimika kuzingatia uzoefu wa watoto anaolenga katika kusoma vitabu, maarifa walionayo, na uwezo wao wa kusoma.

Oittinen (2000), akimnukuu Shavit (1986), anatambua mambo makuu mawili yanayosababisha usilimisho wa kazi kwa ajili ya kusomwa na watoto. Sababu hizo ni: Kwanza, kurekebisha matini chasili ili iweze kuwafaa na kuwa na umuhimu kwa mtoto, huku mwandishi akiongozwa na maadili ambayo jamii inathamini kuwa bora kwa mtoto. Pili, kurekebisha ploti, wahusika na lugha kutoka kwa hali changamano hadi kiwango kinachoweza kufahamika na kueleweka kwa mtoto. Kwa mujibu wa Baker (2001), usilimishaji ni kundi la tafsiri ambazo hutokea katika matini na zinazobadilisha matini hiyo isichukuliwe kama tafsiri bali itambulike kama kiwakilishi cha matini chasili. Hivyo, tunapotathmini usilimishaji katika mtazamo wa kihistoria, tunapata kwamba kuna tofauti kubwa kati ya usilimishaji na tafsiri. Hii ni kwa sababu, tafsiri huwa ni tendo la kushurutisha linalotekelezwa kwa matini chasili. Kwa upande mwingine, usilimishaji ni dhana inayohitaji kutambulisha tafsiri kama kazi ambayo siyo silimisho bali kama mbinu mojawapo ya kubadilisha matini chasili wakati wa usilimisho.

Kulingana na Sanders (2006), dhana ya usilimishaji inatumika kumaanisha kubadilisha, kurekebisha, kuunda na kurahisisha matini chasili ili iweze kueleweka kwa hadhira lengwa. Kwa hivyo, kufupisha na kuunda upya matini lengwa huwa ni

sanaa na mojawapo ya hatua inayozingatiwa katika utaratibu wa usilimishaji. Hatua hii huzingatiwa na mwandishi ili aweze kuibuka na kazi bora inayoeleweka kwa hadhira lengwa.

Kwa ujumla, katika fasihi ya watoto dhana hii hutumiwa kurejelea hali ya kurekebisha au kubadilisha baadhi ya vipengele katika matini chasili kama vile picha, ploti, majina ya wahusika, mtindo wa lugha na maudhui ili kulenga hadhira tofauti na ile iliyolengwa na matini chasili. Katika makala hii, hadithi ya *Elisi Katika Nchi ya Ajabu* (1940) haijatumika kwa sababu imetumia vielelezo tofauti na matini chasili. Badala yake tumetumia hadithi ya *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (2015) kwa sababu imehifadhi vielelezo vya matini chasili. Silimisho la *Wasifu wa Mwana Kupona* (2008) limeteuliwa kwa misingi kwamba, limesilimishwa mara mbili kwa lengo la kufikia hadhira ya watoto. Makala hii imechunguza aina za vielelezo vilivyotumika katika usilimishwaji wa hadithi ya *Wasifu wa Mwana Kupona (*King'ei, 2008) kutoka *Utenzi wa Mwana Kupona* (1972) na *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (Hadjivayanis, 2015) kutoka *Alice's Adventure in Wonderland* (Carrol, 2011) na mchango wake katika kuendeleza ujumbe.

Kusoma na kuchanganua *WMK*[2] (2008) na *ANIA* (2015) ndizo mbinu kuu ambazo zimetumiwa kukusanya data. Katika njia hii ya kukusanya data watafiti wamesoma, kuchambua na kunakili vipengele muhimu vinavyohusiana na vielelezo. Komb na Tromp (2006) wanasema kuwa uteuzi wa kimakusudi wa data unahusu uteuzi wa moja kwa moja wa data yenye sifa zinazolengwa na utafiti husika. Hivyo, matini teule zimechaguliwa kimakusudi. Watafiti wamepitia kwa undani masilimisho teule ili kubainisha aina za vielelezo vilivyotumika katika hadithi ya *WMK* (2008) na *ANIA* (2015). Makala hii ina sehemu tano: utangulizi, nadharia iliyoongoza utafiti, muhtasari wa hadithi teule, aina ya vielelezo vilivyotumika katika hadithi teule na kisha hitimisho.

## 2.0 Misingi ya Nadharia

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Usilimishaji iliyoasisiwa na George Bluestone (1957) na kuendelezwa na Hutcheon (2013). Kulingana na Hutcheon, hadithi huwa mhimili mkuu wa usilimishaji kwa sababu harakati ya usilimishaji hujikita kwenye hadithi husika. Hivyo basi, vihadithi katika hadithi kuu vinaweza vikafupishwa na hata msuko wake kufaraguliwa. Aidha, mwendo wa hadithi unaweza kuumbwa upya, muda ukafinywa ama kunyambuliwa. Hata hivyo, haiwezekani kuubadilisha mtazamo wa hadithi, kwa sababu kufanya hivyo

[2] Kwa kifupi *Wasifu wa Mwana Kupona* tutaandika *WMK* (2008), *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* tutaandika *ANIA* (2015), *Utenzi wa Mwana Kupona* tutaandika *UM* (1972) na *Alice's Adventures in Wonderland* tutaandika *AWW* (2001).

kunaweza kuzalisha hadithi mpya. Mhimili huu umesaidia kubainisha aina za vielelezo vilivyotumika katika hadithi ya *WMK* (2008) na *ANIA* (2015) na mchango wake katika kuendeleza ujumbe.

### 3.0 Muhtasari wa *Wasifu wa Mwana Kupona*

Kitula King'ei ameusilimisha *Utenzi wa Mwana Kupona* mara mbili. Aliusilimisha mara ya kwanza mwaka 2000 katika Kiingereza na kuuita *Mwana Kupona: Poetess from Lamu* (2000). Baadaye, aliusilimisha utenzi huohuo mwaka 2008 katika Kiswahili na kuuita *Wasifu wa Mwana Kupona* (2008).

Hadithi ya *Mwana Kupona: Poetess from Lamu* (2000) ni kisa cha kusisimua ambacho kimeelezwa kupitia dayolojia, vichekesho na hata mtiririko wa vitushi vya hadithi. Hadithi ya *Mwana Kupona; Poetess from Lamu* (2000) imejengwa na maudhui ya mapenzi, maisha, dini ya Kiislamu na hata sehemu za shairi kutoka *Utenzi wa Mwana Kupona* (1972). Aidha, hadithi hii imeshugulikia utunzi wa ushairi wa Kiswahili na hata maisha ya Lamu. Mathalan, vielelezo vimetumika katika baadhi ya kurasa labda kwa lengo la kusisitiza yale yaliyoandikwa kwenye matini. Hadithi ya *Mwana Kupona: Poetess from Lamu* (2000) ni faafu kwa watoto na hata watu wazima.

Silimisho la pili la *Wasifu wa Mwana Kupona* (2008) sawia na *Mwana Kupona: Poetess from Lamu*, limejengwa kwa vielelezo vilivyotiwa rangi na maandishi katika matini. Hadithi ya *Wasifu wa Mwana Kupona* (2008) imejengwa na maudhui ya ndoa, nafasi ya mwanamke, mapenzi, dini ya Kiislamu, urafiki miongoni mwa maudhui mengine. Maudhui yamejengwa kupitia wahusika kama vile Mwana Kupona, Zuhura, Mwana Hashima, Abu, Mohammed miongoni mwa wahusika wengine. Mwisho, ni wazi kwamba masilimisho yote mawili yaani *Mwana Kupona: Poetess from Lamu* (2000) na *Wasifu wa Mwana Kupona* (2008) yalimlenga mtoto tofauti na *Utenzi wa Mwana Kupona* (1972) ambao ulimlenga mwanamke aliyekuwa tayari katika ndoa.

### 3.1 Muhtasari wa *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu*

Charles Lutwidge Dodgson ndiye mwandishi halisi wa kitabu cha *Alice in Wonderland* (1865). Charles Lutwidge pia anafahamika kama Lewis Carroll (Hadjivayanis, 2015). Riwaya ya *Alice in Wonderland* (1865) ni miongoni mwa vitabu vya fasihi ambavyo vimesilimishwa na kutafsiriwa sana. Hii ina maana kwamba, watafiti wengi wanaweza kujifunza lugha nyingi zilizotumika kutafsiri riwaya ya *Alice in Wonderland* (1865). Tangu kutungwa kwa riwaya ya *Alice in Wonderland*, kuna takriban tafsiri 174 ambazo zimefanywa katika lugha mbalimbali za ulimwengu pamoja na lahaja zake. Baadhi ya lugha ambazo zimetafsiri riwaya ya *Alice in Wonderland* (1865) kutoka Kiingereza hadi lugha zingine ni Kiarabu, Kijapani, Kikorea na Kiswahili.

Kulingana na Hadjivayanis (2015) hadithi ya *Alice in Wonderland* (1865) imetafsiriwa na kusilimishwa katika Kiswahili mara mbili. Silimisho na tafsiri ya kwanza inafahamika kama *Elisi Katika Nchi ya Ajabu* (1940). Riwaya hii ya *Elisi Katika Nchi ya Ajabu* (1940) ilitafsiriwa na kusilimishwa kwa mara ya kwanza katika Kiswahili mnamo mwaka 1940 na Ermyntrude Virginia St Lo de Malet ambaye pia anafahamika kama Conan-Davies. Saint Lo alikuwa mmishenari na pia mfasiri wa Kiingereza hadi Kiswahili. Mathalan, katika karne ya 19, tafsiri ilikuwa ndiyo chanzo cha riwaya katika fasihi ya Kiswahili na hivyo basi ikaweza kuathiri waandishi wa wakati ule. Katika tafsiri yake ya *Elisi Katika Nchi ya Ajabu* (1940), Saint Lo alibadilisha mandhari ya hadithi kutoka yale ya Uingereza hadi yale ya Afrika Mashariki na pia kumgeuza mhusika mkuu kuwa mtoto wa Kiafrika na kumuita Elisi. Mhusika Elisi alisawiriwa kama mtoto wa Kiafrika kwani alitembea bila viatu, alivalia nguo za khanga na hata kusuka nywele zake tofauti na Alice wa Uingereza. Hadjivayanis (2015) anaongeza kwamba, alimgeuza mhusika mkuu Elisi ili kumweka karibu zaidi na ukweli wa maisha ya watoto wa Kiswahili ambao hawakuwa na ujuzi mkubwa wa utamaduni na maisha ya watoto wa Kizungu. Isitoshe, hadithi ya Elisi haina mambo mengi ya Kiulaya lakini kijumla kuna mambo mengi ya Kizungu kwa mfano mnyama kama vile *Gryphon* na vyakula kama *treacle, tarts, pies* na *marmalade*.

Silimisho na tafsiri ya pili ya hadithi ya *Alice in Wonderland* (1865) ilifanywa na Ida Hadjivayanis mnamo mwaka 2015 kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Silimisho na tafsiri ya Ida Hadjivayanis iliitwa *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (2015) na lilitolewa kama mojawapo ya kazi zilizosherehekea kutimia kwa miaka 150 tangu kuchapishwa kwa toleo la kitabu hiki mwaka 1865. Tafsiri na silimisho hili linanuia kumwezesha msomaji wa *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (2015) kupata hisia zilizokusudiwa na mwandishi wa hapo awali.

## 4.0 Vielelezo katika Fasihi ya Watoto

Kwa mujibu wa Hunt (2006) vielelezo ni vipengele ambavyo hutumika kuwasilisha ujumbe changamano hasa kwa kusawiri vitu halisi kutoka kwa jamii au ulimwengu halisi. Hunt (2006) anaongeza kwamba vielelezo ni vipengele muhimu vya kuwasilisha ujumbe tofauti na njia ya maandishi katika matini ambayo imezoeleka kwa wengi. Naye Sever (2012) anaeleza kwamba vielelezo ni ujumi unaochochea uundaji wa ujumbe na unafafanua kwa kina maana ya maandishi yaliyoko kwenye matini. Kutokana na maoni ya wataalamu hawa, ni dhahiri kwamba vielelezo ni vipengele ambavyo hutumika kupasha ujumbe katika matini na hivyo basi huingiliana kwa lengo la kupitisha ujumbe husika. Kwa mujibu wa Kiefer, Helper na Hickman (2007) vielelezo ni vifaa vya kimsingi vinavyotumika kufunzia watoto

katika fasihi ya watoto. Wachoraji hutumia aina mbalimbali ya vielelezo kama njia ya kuwasilisha ujumbe katika fasihi ya watoto.

### 4.1 Aina ya Vielelezo Vilivyotumika katika Hadithi Teule

Katika kusilimisha kazi teule, vielelezo mbalimbali vimetumiwa. Mifano ya vielelezo vilivyotumiwa katika sehemu hii imetolewa kutoka kwa silimisho la *Wasifu wa Mwana Kupona* (2008) na *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (2015). Matini asilia iliyotumiwa kusilimisha vitabu hivi ni *Utenzi wa Mwana Kupona* (1972) na *Alices Adventure in Wonderland* (2011).

#### 4.1.1 Vibonzo

Mifflin (2009) anaeleza kuwa neno kibonzo linatokana na neno la Kifaransa *Cartoon* (mchoro), Kiitaliano *Cartone* na Kidachi *Karton* linalomaanisha karatasi nzito au ngumu. Katuni ni ubao wa kuchora mchoro mzima kwa rangi kwenye karatasi ngumu iliyo kama kielelezo cha kusoma ambacho huitwa *modello* (Kilatini). Kutokana na maana hii asilia, neno kibonzo limechukua maana tofauti tofauti. Hata hivyo, kutegemea miundo au maumbo na matumizi yake katika jamii, wataalamu mbalimbali wameweza kufafanua dhana ya kibonzo kwa namna tofauti. Kwa mfano, Lester (1987) anasema kuwa kibonzo ni mchoro au picha inayowasilishwa na kusimamia muundo fulani unaoonesha umbo fulani na umuhimu wake katika hadithi. Kulingana na Kimani (2006), vibonzo hujitokeza katika michoro, picha au vielelezo na huwa ni maumbo ya kuchekesha. Otuoma (2012) anasema kwamba kuna aina tatu za vibonzo; vibonzo vya michoro, vibonzo vya filamu na vibonzo vya paneli. Katika makala hii, tutajadili vibonzo vya paneli kama vilivyotumika katika vitabu teule.

Lordan (2006) na Otuoma (2012) wanasema kuwa vibonzo vya aina ya paneli huwa kwenye paneli moja ili kuweza kutoa hadithi fulani inayosisimua, lakini kwa mtazamo wa yanayofanyika katika jamii kila uchao. Kila mara huwa na kinachochochea wasomaji wake chini ya paneli hiyo. Kwa mfano, *Bogi Benda* na *Phantom na Spiderman*. Isitoshe, vitabu vya aina hii huwa na mwendelezo wa hadithi, kama vile *Tin Tin, Pink Panther* miongoni mwa hadithi nyinginezo. Otuoma (2012) anasema kwamba, vibonzo ni mojawapo wa *Zeitgeist* (kipindi cha mapinduzi) na kwa kuvitazama huwa vinaleta dhana ya *Zeitgeist* wakati vinapochapishwa na hivyo basi, vibonzo vya miaka kati ya 1950 hadi 1959 vinatuelezea jinsi ambavyo ukoloni ulivyoendelezwa.

Hadithi ya *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (2015) imetumia vibonzo vya aina ya paneli ili kuelezea mtiririko wa ploti ambao ni wa kufurahisha kwa hadhira ya mtoto. Tazama mfano wa *ANIA* (2015: 8).



**Chanzo:** *ANIA* (2015: 8)

Katika kielelezo hiki, kuna mhusika Sungura ambaye amevalia koti huku akiwa amekamata saa mkononi na pia kuweka mkono wake kwapani. Sungura huyu amesimama katika mazingira ambayo kuna mimea na anaonekana kana kwamba anaangalia saa yake. Katika kielelezo hiki cha *ANIA* (2015: 8) mhusika Alisi alikuwa amemwona Sungura ambaye alikuwa anaangalia saa yake na hivyo basi Alisi akaamua kumfuata na katika harakati hiyo, Sungura alikimbia huku akimwambia Alisi kuwa hana muda. Alisi hakumsikiliza Sungura na badala yake aliendelea kumkimbiza hadi pale Sungura alipokimbilia ndani ya shimo. Alisi alimfuata Sungura kwenye shimo na kuanza kuchungulia mle ndani na kwa bahati mbaya, alitumbukia mle ndani na kuanguka kwa kishindo.

Kielelezo hiki kimetumika kuwasilisha maudhui ya uhalisia wa ajabu kwani mhusika sungura ambaye ni mnyama ana uwezo wa kuzungumza na binadamu na hata kuvalia nguo kama vile binadamu. Alisi pia ana uwezo wa kuzungumza na wanyama na hata kuanguka ndani ya kisima kirefu bila ya kuumia. Mchoraji wa *ANIA* (2015: 8) hakuona haja ya kubadilisha kielelezo hiki kutoka matini chasili.

**4.1.2 Ramani**

Kando na kielelezo cha paneli, wachoraji hutumia ramani kama njia ya kupasha ujumbe. Kulingana na Kümmerling-Meibauer na Meibauer (2015) ramani hutumika kama ishara ya viwakilishi na pia kurembesha kazi ya watoto. Lengo kuu la ramani huwa ni kusaidia katika uelewa wa hadithi katika fasihi ya watoto. Goga na Kümmerling-Meibauer (2017) wanaeleza kuwa ramani ni kifaa ambacho hutusaidia kupanga, kuweka na kukumbuka habari kuhusu eneo fulani. Goga na Kümmerling-Meibauer (2017) wanaongeza kwamba, tafiti ambazo zimefanywa kuhusu historia na maendeleo ya ramani katika fasihi ya watoto ni chache na si za kina.

Kulingana na Pavlik na Bird (2017), ramani katika fasihi ya watoto zinaweza kuwekwa katika makundi matatu. Kwanza, ramani ambazo husawiri mandhari halisi. Pili, ramani za kifantasia ambazo hazina uhalisia wowote na

zimebuniwa na msanii. Tatu ni ramani ambazo zinahusu uhalisia na ufantasia kwa wakati mmoja. Pavlik na Bird wanaongeza kwamba ramani zilitumika katika kazi za watoto kama vielelezo tangu mwaka 1882 wakati ambapo Robert Louis Stevenson alipotumia ramani katika kitabu chake cha *Treasure Island.* Ramani ni aina ya kielelezo ambacho kimepuuzwa na wahakiki wa kazi za watoto. Awali, vitabu vya watoto vilivyokuwa na ramani vilichukuliwa kuwa vitabu vya watoto wa kiume. Siku hizi, watoto wana maarifa kuhusiana na masuala ya ramani na hii ni kwa sababu ya ufunzaji wa somo la Jiografia shuleni (Pavlik na Bird, 2017). Kulingana na Kümmerling-Meibauer na Meibauer (2015) ramani hutumika kutoa muhtasari wa hadithi hasa kuhusu masuala ya mandhari, wakati na uhusiano wake katika hadithi. Katika kielelezo hiki cha *WMK* (2008:72) kuna ramani ambayo imechorwa ili kuonyesha baadhi ya sehemu mbalimbali za pwani. Mtunzi wa *WMK* (2008) aliweka kielelezo hiki ili kumwonyesha msomaji baadhi ya sehemu ambazo Mwana Kupona alipitia alipokuwa katika safari yake ya kutoka Lamu kwenda Pate kumsalimia rafiki yake Fatuma. Ramani hazijatumika katika *UM* (1972), *ANIA* (2015) wala *AAW* (2011). Matumizi ya ramani yapo kwenye silimisho la *WMK* (2008), tazama mfano wa *WMK* (2008:72**)**.




**Chanzo:** *WMK* (2008: 72)

Kielelezo hiki cha *WMK* (2008:72) kimetumika kuwasilisha maudhui ya mandhari ya pwani. Sehemu zilizoorodheshwa katika kielelezo hiki zipo katika maeneo ya pwani na hivyo basi, msomaji anapokitazama anapata taswira ya jinsi miji inavyofuatana katika eneo hili. Maudhui haya ya mandhari ya pwani yapo katika *UM* (1972) japo hayajawekwa katika kielelezo kama alivyofanya mtunzi wa *WMK* (2008).

### 4.1.3 Picha za Rangi

Picha zilizotiwa rangi hutumiwa kwa wingi katika hadithi za watoto. Cass (1984) anasema kwamba, watoto huchagua vitabu vilivyo na mng'aro wa hali ya juu. Kauli

hii imesisitizwa na Tucker (1984) ambaye anaongeza kuwa, rangi ni kipengele muhimu katika vitabu vya watoto wadogo. Watoto hupendelea vitabu ambavyo vina picha iliyotiwa rangi. Watoto huchagua vitabu vilivyo na picha nyeusi au nyeupe iwapo hadithi hiyo wanayosoma inafurahisha. Watoto hutambua kwa urahisi rangi nyekundu ikifuatiwa na rangi ya manjano, samawati na kisha kijani. Katika kazi za watoto rangi inaweza kutumika kumtisha mtoto au hata kumbembeleza hasa kwa kutegemea jinsi picha ilivyotumia rangi. Watoto hunasibisha rangi na mambo mbalimbali kama vile jua-manjano, wingu-samawati, nyasi-kijani na shina-hudhurungi. Aidha, Wills (2015) anaongeza kuwa, kitu cha kwanza ambacho watoto hufurahia na hata kuonyesha hisia kwayo ni rangi.

Kulingana na Wills (2015) vielelezo vilivyotiwa rangi katika kazi za watoto ni muhimu na huchangia kwa njia mbalimbali katika fasihi ya watoto. Kwa mfano, iwapo rangi itatumika vizuri katika kazi za watoto, basi huenda ikawafanya kuwa na utashi wa kusoma na hivyo kukua kiakili. Pili, rangi angavu zinapotumiwa vizuri na wasanii katika kazi za watoto huwafanya watoto kujinasibisha na yale wanayosoma na mambo wanayoyaona katika ulimwengu halisi. Vilevile, picha zilizotiwa rangi tofauti tofauti zina maana kwa watoto kwa sababu huwasaidia kutofautisha mambo halisi na yale ya kifantasia. Kwa mfano, mti wa mchungwa ambao una shina lenye rangi ya zambarau utazua mdahalo baina ya watoto na mwisho, rangi humwezesha mtoto kutambua mazingira na hivyo basi kumpa nafasi ya kuelewa anakoishi.

Fox (1985) na Ruthiiri (2012) wanakubaliana kwamba uhakiki wa kitabu cha watoto huanzia katika jalada na kwa hivyo jalada hubeba ujumbe kwa muhtasari wa hadithi iliyomo ndani ya kitabu. Ujumbe kwenye jalada unahitaji kuwa wenye mvuto. Katika fasihi ya watoto, vielelezo kwenye jalada huweza kuwa ndicho kigezo kinachompa mtoto motisha ya kusoma kitabu fulani. Pia, rangi iliyo kwenye jalada la kitabu cha watoto yapaswa kuwa angavu na ya kuvutia. Kiungo muhimu kabisa katika umbo la kitabu ni vielelezo au ule uwasilishaji wa maneno kwa kutumia picha. Katika fasihi ya watoto hasa watoto wa kiwango cha chini, vielelezo husadia sio tu kukifanya kitabu kivutie machoni mwa mtoto, lakini pia husisitiza dhana muhimu katika kitabu. Mathalan, vielelezo huwasaidia wasomaji ambao uelewa wao wa dhana ni wa kiwango cha chini. Kimsingi, vielelezo husaidia kueleza matini au hadithi, kuleta mvuto kwa msomaji, kueleza kwa muhtasari wazo kuu, kusaidia kuondoa uchovu wa msomaji, kumsaidia mtoto kukumbuka hadithi na hata kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu sehemu ya hadithi.

Picha zilizotiwa rangi zimetumika katika majalada yote ya masilimisho teule, yaani *WMK* (2008) na *ANIA* (2015) katika uundaji wa ujumbe wake. Picha za rangi pia zimetumika kwa wingi katika silimisho la *WMK* (2008). Tazama mfano wa jalada la mbele kutoka *WMK* (2008).



**Chanzo:** *WMK* (2008) (Jalada la mbele)

Kwa kutazama kielelezo hiki cha *WMK*, mtazamaji anapata taswira kamili ya mandhari ya eneo la pwani. Kuna mwanamke ambaye amekaa chini ya mnazi huku akiwa amezama katika uandishi wa utenzi hasa kwa kutazama mada yake. Mwanamke huyu amekaa kando ya bahari na mimea iliyoko katika mazingira haya ni ya kijani kibichi huku miti mingi katika picha hii ikiwa ni minazi ambayo matunda yake yanaonekana yakining'inia. Mwanamke ambaye amezama katika utunzi wa utenzi katika kielelezo hiki ni Mwana Kupona. Mwana Kupona amejifunika hijabu nyeupe na kuvalia rinda la rangi ya waridi. Vilevile, kando yake kuna jumba la kifahari. Mandhari yanayosawiriwa katika *WMK* yanawasilisha utamaduni wa Waswahili hasa kutokana na mimea, bahari, mavazi na hata lugha ya Kiswahili ambayo mtunzi anaitumia katika utunzi wake.

Kielelezo cha *WMK* kimetumika kuwasilisha maudhui ya utamaduni wa Uswahilini na nafasi ya mwanamke katika elimu. Kujitosa kwa mwanamke katika utunzi wa utenzi ni ushahidi kwamba mwanamke Mswahili anapigania nafasi sawa na ile ya mwanaume katika ulimwengu wa elimu. Kauli hii inaingiliana na mawazo ya waasisi wa Nadharia ya Ufeministi ambao wanasema kuwa nadharia hii inanuia kuwasawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana (Njogu na Chimerah, 1999). Katika matini chasili ya *UM* (1972) hakuna kielelezo cha mwanamke ambaye anajihusisha na utunzi wowote lakini kutokana na ubeti wa tatu kutoka *UM* (1972) msomaji anapata uelewa kwamba kazi lengwa imetungwa na mwanamke ambaye ana lengo la kumpa mwanawe mawaidha, kama ubeti ufuatao unavyoeleza.


**Ubeti wa 3**

Ndoo mbee ujilisi
Na wino na qaratasi
Moyoni nina hadithi
Nimepanda kukuambia

**Chanzo:** *UM (*1972:123)

Katika kielelezo cha *WMK* mchoraji ameusawiri ubeti huu kwa kutumia karatasi na wino ili kuonesha vifaa ambavyo Mwana Kupona alivitumia katika utunzi wa *UM* (1972).

Aidha, katika jalada la mbele la *ANIA* (2015), kuna sungura ambaye amevalia rinda ambalo limechorwa maua ya ishara ya upendo. Mkononi ameshika karatasi na mdomoni anaonekana kupuliza tarumbeta huku jalada likikolezwa kwa rangi ya waridi. Kuna mada ambayo pia imeandikwa kwenywe jalada '*Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu'*. Sungura aliyesawiriwa hapa ni yule aliyekuwa akiongoza mijadala katika mahakama katika kisa *ANIA* (2015). Tazama kielelezo kifuatacho:





**Chanzo:** *ANIA* (2015) (Jalada la mbele).

Maudhui yanayojengwa katika kielelezo hiki ni ya safari. Alisi yuko mbioni kumsaka Sungura Mweupe na hivyo kisa hiki kina wahusika wawili wakuu yaani; Alisi na Sungura Mweupe. Alisi amejikuta katika ulimwengu wa ajabu kwa sababu ya kumfuata mhusika Sungura. Kielelezo hiki kinakubaliana na mawazo ya Smith, Goodman na Meredith (1970) ambao wanasema kwamba, vielelezo vinavyotumika kwenye jalada ni muhimu sana na vinafaa vichorwe kwa umakini ili viingiliane na anwani ya kitabu na yaliyomo. Kisa cha Alisi ni cha kumsaka Sungura na hivyo basi kielelezo hiki kinaingiliana na matini.

### 4.1.4 Michoro

Aina nyingine ya vielelezo ambavyo hutumika ni michoro. Kwa mujibu wa TUKI (2006:641), mchoro ni picha, ramani, vielelezo au taswira. Mchoro ni uzalishaji wa vielelezo kiusanii kama vile kwenye karatasi huku ukitumia wino, chaki au hata makaa. Isitoshe, mchoro unaweza kuwa umbo au kielelezo cha kilichochorwa kwa haraka ili kuwasilisha ujumbe kwa njia sahili. Mchoro ni vielelezo ambavyo ni rahisi kuchora na huweza kuwasilishwa kwa hadhira ya watoto kwa njia sahili kabisa. Mchoro wa *WMK* (2008: 16) umetumiwa na mchoraji ili kusisitiza maudhui ya dini ya Kiislamu ambayo yameshamiri katika *UM* (1972). Mchoro huu unaonesha kielelezo cha Korani Tukufu. Katika beti za 101 na 102 mtunzi wa *UM* (1972) amemaliza utungo kwa kutoa dua kwa Maulana kama wafanyavyo watunzi

wa tenzi nyingi za Waswahili, wakiwemo Waislamu. Tazama mfano wa mchoro huo na beti hizo:




**Chanzo:** *WMK* (2008: 16)

**<u>Ubeti wa 101</u>**

Mola tatusahilia
Kwa Baraka za Nabia
Na masahaba pamoya
Dini waliotetea

**<u>Ubeti wa 102</u>**

Nahimidia kisalia
Kwa tume wetu nabia
Ali zake na dhuria
Itwenee sote pia.

**Chanzo:** *UM* (1972:140)

Beti hizi zinamsifu Mwenyezi Mungu kwa misingi ya dini ya Kiislamu. Katika *WMK* (2008) suala la dini ya Kiislamu limeshughulikiwa kwa mfano, kwa kutazama kielelezo cha *WMK* kuna maandishi katika kielelezo hiki ambacho kinawiana na Korani Tukufu. Maandishi katika Korani huandikwa kwa Kiarabu hasa kutoka kulia kwenda kushoto. Japo mada katika kielelezo hiki imetumia Kiswahili, huenda maandishi mengine yameandikwa kwa kutumia Kiarabu. Matini chasili ya *UM* (1972) haikutumia kielelezo chochote kupitisha maudhui kama ilivyo katika silimisho la *WMK* (2008). Katika kielelezo cha *WMK* (2008: 16) mchoraji anafafanua baadhi ya beti za *UM* (1972) kama vile ubeti wa 94 na ule wa 95 ambapo Mwana Kupona anamwambia Mwana Hashima ni vyema kumtii mumewe na kufuata kaida za dini ya Kiislamu.

**<u>Ubeti wa 94</u>**

Somani nyue huramu
Maana muyafahamu
Musitukue laumu
Mbee za Mola Jalia

**<u>Ubeti wa 95</u>**


Somani mite ya nganu
Mutii waume wenu
Musipatwe na zitunu
Za akhera na dunia

**Chanzo:** *UM* (1972:138)

Hivyo, katika kielelezo cha *WMK* (2008: 16) mchoraji amefanikisha kuunda maudhui ya dini ya Kiislamu kwani Mwana Kupona anamwambia Mwana Hashima kuwa mafunzo yaliyomo katika Korani Tukufu ndiyo msingi na mwongozo wa maisha ya binadamu. Anaongeza kwamba Korani Tukufu ni mapenzi ya Mungu juu ya maisha ya binadamu na binadamu hana budi kuyatii. Kutokana na kielelezo hiki

cha *WMK* (2008: 16) ni dhahiri kwamba maandishi yanaweza kusilimishwa kupitia vielelezo ili kulenga hadhira nyingine tofauti na kubeba ule ujumbe ulionuiwa.

Aidha, kimetumika kielelezo mchoro kupitia shairi katika *ANIA* (2015: 31). Wamitila (2003) anaeleza kuwa shairi ni utungo ambao una mistari iliyogawika katika mafungu kadhaa. Utungo huu unaweza kuwa na mpangilio unaoonesha mfuatano maalum wa silabi hizo. Hata hivyo, inawezekana mpangilio wake ukawa huru.


"Ghadhabu alimwambia
panya, Ambaye aliku-
tana naye ndani
ya nyumba, 'Sisi
sote wawili twende
katika sheria:
Mimi nitaku-
shtaki *wewe*.—
Njoo, Mimi
sitakubali
kukanwa:
sisi Lazima
tuwe na kesi;
Kwani kweli
Asubuhi hii
Mimi sina
Chochote
Cha kufanya.'
Alisema
Panya kwa
Mbwa koko,
'Kesi kama
hiyo, bwana
mpendwa.
Bila ya
Wajumbe Wa
baraza la
mahakama
au jaji,
itakuwa
kupoteza
pumzi
yetu.'
'Nitakuwa
jaji,
nitakuwa
ujumbe'
alisema
Mjanja
Gha-
dhabu:
Nita
jaribu
sababu
yote
na,
kuku-
hukumu
hadi
kifo.'

**Chanzo:** *ANIA* (2015: 31)

Kulingana na Onyancha (2015) ushairi huru ni aina ya ushairi usiozingatia arudhi za wanamapokeo. Onyancha anaongeza kwamba ushairi mchoro ni pale ambapo watunzi wanatumia maumbo ya dhana ya kitu wanachokishughulikia kimaudhui. Mchoro wa *ANIA* (2015: 31) umetumika kuwasilisha ujumbe japo kwa njia ya ushairi wa picha. Mchoro huu unafanana na mkia wa panya. Kielelezo hiki cha *ANIA* (2015: 31) kimetumika pia katika *AWW* (2011) na kimefanikisha kuunda maudhui ya masaibu yaliyompata panya.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imebainisha namna ambavyo usilimishwaji wa vibonzo umetekelezwa katika vitabu teule vya watoto kwa kuonesha aina nne za vielelezo vilivyotumiwa. Aina hizi ni vibonzo, ramani, picha zilizotiwa rangi na michoro. Aina ya kielelezo ambacho hakijatumiwa katika masilimisho teule ni ile ya sanamu. Kutokana na makala hii, ni wazi kwamba vielelezo vinaweza kutumika kuunda, kupasha ujumbe kwa mtoto anayesoma hadithi na kuchangia katika kuelewa hadithi hiyo.

## Marejeleo


Andrew, D. (1984). *Concepts in Film Theory*. New York: Oxford University Press.

Baker, M. (2001). *Routledge Encyclopedia of Translation Studies*. London: Philadelphia Routledge.

Balodis, J.M. (2012). The Practice of Adaptation: Turning Fact and Fiction into Theatre. (Unpublished) PhD Thesis, Queensland University of Technology.

Bluestone, G. (1957). *Novels into Film*. Berkeley: University of Berkeley.

Bohl, A. (1997). *Guide to Cartooning*. Gretna: Pelican Publishing.

Brisset, A. (1990). *Sociocritique of Translation Theature*. New York: Routledge.

Carroll, L. (1940). *Elisi Katika Nchi ya Ajabu.* London: Sheldon Press.

Carroll, L. (2011). *Alice's Adventures in Wonderland*. Peterborough: Broadview Press.

Cass, J.E. (1984). *Literature and the Young Child*. London: Longman Group Ltd.

Feldman, O. (2005). *Talking Politics in Japan Today*. Brighton: Brighton Sussex Academics Press.

Fox, G. (1985). *Teaching Literatubre: Nine to Fourteen*. New York: Oxford University Press.

Goga, N. and Kümmerling-Meibauer, B. (Eds.). (2017). Maps and Mapping in Children's Literature: Landscapes, Seascapes and Cityscapes (Vol. 7). Retrieved from https://benjamins.com/catalog/clcc. October 11, 2019.

Goodman, N. (1976). *Languages of Art.* Indianopolis: Hacket.

Hadjivayanis, I. (2015). *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu*. Portlaoise: Everytype.

Hunt, P. (2006). "Introduction: The Expanding World of Children's Literature Studies." In P. Hunt (Ed.) *Understanding Children's Literature* (pp. 11-24). New York: Routledge.

Hutcheon, L. (2013). *A Theory of Adaptation.* New York: Routledge.

Kaui, T.M. (2011). Tathmini ya Usilimisho wa Riwaya na Hadithi Fupi kwa Wanafunzi wa Sekondari Nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kiefer, B.Z., Hepler, S. and Hickman, J. (2007). *Charlotte Huck's Children's Literature.* New York: The McGraw-Hill Companies.

Kimani, H.W. (2006). Uwiano wa Picha na Matini katika Mabango ya Matangazo ya UKIMWI: Mtazamo wa Kisiomitiki. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

King'ei, K. (2000). *Mwana Kupona: Poetess from Lamu.* Nairobi: Sasa Sema Publishers limited.

King'ei, K. (2008). *Wasifu wa Mwana Kupona*. Nairobi: Sasa Sema Publishers Limited.

Klingberg, G. (1986). *Children's Fiction in the Hands of the Translators*. Risskov: Gleerup.

Komb, D. K. and Tromp, L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction.* Nairobi: Paulines Publications.

Kümmerling-Meibauer, B. and Meibauer, J. (2015). "Maps in Picturebooks: Cognitive Status and Narrative Functions." *Barnelitterært Forskningstidsskrift*. Pp. 1-4.

Lester, M. (1987). *Political Cartoons Editorial News*. Rome: News Tribune.

Lordan, E. J. (2006). *Politics, Ink: How America's Cartoonists Skewer Politicians, from King George III to George Dubya*. Maryland: Rowman & Littlefield.

Mifflin, H. (2009). *The Best American Comics.* New York: Amazon.

Muthubi, F. (2005). Mikakati na Mbinu za Usilimishwaji katika Fasihi ya Watoto. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation* (Vol. 66). New York: Prentice hall.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Obonyo, L. (2004). "Cartoonists in Kenya: Past Present and Future." *International Journal of Comic Art.* 96-116.

Omuya, R. (2017). Usilimishwaji wa *Biblia* kama Fasihi ya Watoto: Hadithi Teule. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Onyancha, J. W. (2015). Changamoto za Mikondo Mipya ya Utunzi wa Mashairi ya Kiswahili: Mfano wa *Tunu ya Ushairi*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Otuoma, D. A. (2012). Mitindo na Maudhui katika Uchanganuzi wa Vibonzo kwenye gazeti la *Taifa leo*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Pavlik, A. and Bird, H. S. (2017). "Introduction: Maps and Mapping in Children's and Young Adult Literature." *Children's Literature in Education*. 1-5.

Ratiba, B. (2014). Adaptation in Translating Children's Literature. Unpublished Masters Thesis. University of Kasdi Merbah Ouargla.

Ruthiiri, M.K. (2012). Tathmini ya Ufaafu wa Vitabu vya Kusoma kwa Madarasa ya 5 na 6 katika Shule za Msingi: Mifano ya Waandishi Wanne. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sanders, J. (2006). *Adaptation and Appropriation: New Critical Idiom*. London: Routlege.

Sever, S. (2012). *Children and Literature*. Izmir: Tudem.

Schallert, D. L. (1980). The Role of Illustrations in Reading Comprehension, *Theoretical Issues in Reading Comprehension*. 503-524.

Shavit, Z. (1986). *Poetics of Children's Literature*. Athens: Georgia University Press.

Sheikh, A.A. na Nabhany, A.S. (1972). *Utendi wa Mwana Kupona: Utendi wa Ngamia na Paa*. Heinemann Educational Books.

Sohaimi, A. (2011). *Adaptation of Hikayat Hang Tuah in Children's Literature*. Malaysia: University of Utara.

Starrs, D. B. (2006). "A Queer New World: Adaptation Theory and the Zeugma of Fidelity in Derek Jarman's *The Tempest.*" The University of Melbourne, Vol. IV. Issue 1.http://docs.google.com. Imesomwa Julai 27, 2018.

Tucker, N. (1984). *The Child and the Book: A Psychological and Literary Exploration*. Cambridge: Cambridge University Press.

TUKI (2006). *English-Swahili Dictionary*. Dar es Salaam: TUKI.

Oittenen, R. (2000). *Translating for Children*. New York. Garland Publishing, Inc.

Vinay, J. na Darbenet, P. (1958). *Translation Procedure and Strategies*. London: Routledge.

Wills, S. (2015). The Childrens Books. https://www.happydesigner.co.uk. Imesomwa Aprili 22, 2019.